**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**6 Novemba 2024**

# TAARIFA KWA UMMA

Taarifa inatolewa kwa umma kuwa kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 30(1)(a) cha *Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006*, Benki Kuu ya Tanzania imeridhia ombi la uunganishaji wa benki mbili za kijamii, yaani Kilimanjaro Co-operative Bank Limited na Tandahimba Co-operative Bank Limited na kuunda benki moja mpya inayojulikana kama Co-operative Bank of Tanzania Limited. Kufuatia muunganiko huo, Benki Kuu ya Tanzania imetoa leseni ya kufanya biashara ya kibenki kwa Co-operative Bank of Tanzania Limited kuanzia tarehe 4 Oktoba 2024. Leseni hii inairuhusu benki kufanya biashara kama benki ya biashara inayoruhusiwa kutoa huduma za kibenki katika mikoa yote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Makao makuu ya benki hiyo mpya yapo katika Kiwanja Na. 21 kitalu Na. 13, Mtaa wa Kuu, Dodoma.

**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**